# TEGA SIKIO UJIFUNZE –EPISODE 10

## ' Kwa nini tunapendana'

**Mwandishi :** Christine Watty
**Mwelekezi** : Maja Dreyer
**Tafsiri** : Anne Thomas/Eric Ponda

**Wahusika**

Mtangazaji
Jenny
Jack
Nele (Binamuye Jenny, miaka 7)
Nyanyake Jenny
Tom (kakake mkubwa Jack)

**Atmos na Sauti:**

'Nje ya shule' sauti za watoto/ magari yanapita/ ndege wanaimba, hatua (Jack anatembea)
Familia yasherehekea, watu wengi wakifurahia burudani, muziki, hali ya utulivu, hatua (Nele anakuja mbio)
Mlango unabishwa, mlango wafunguliwa, sauti ya mtu akiketi kitandani, mtu anaenda miayo na kujinyoosha (Jack) muziki au redio ikisikika taratibu kwa mbali, shuka za kitanda zikigusana, chumbani, akiandika ujumbe katika simu ya mkono, mlango wafungwa
Mchezo wa kandanda, mpira wamgonga Jack kichwani, hatua (Jenny anakuja mbio)

**INTRO (Mtangazaji)**

Karibu tena msikilizaji katika mchezo mwingine wa kuigiza wa redio katika mfululizo wa vipindi kwa jina Kujifunza kwa Kusikiliza,elimu ya Kawaida'. Katika makala ya leo, ambayo pia ni ya mwisho, tunazungumza kuhusu 'mapenzi'. Na kama ilivyo kawaida mapenzi hutatanisha – hasa kwa wana-sayansi wetu chipukizi,- Jack na Jenny. Wote wawili wanahisi zile dalili za kawaida za kuhisi mapenzi – kama vile moyo kwenda mbio, kujisikia mgonjwa, kisunzi. Je wanamapenzi? Kama ndiyo, na nani? Lakini hadi sasa wamekuwa marafiki wakubwa tu, au sivyo? Tunatumai kwamba utaipenda makala hii maalum kuhusu ni kwa nini tunapendana....

1.SCENE:

*'Nje ya shule' kwa nyuma tunasikia sauti za watoto / magari yanapita / ndege wanaimba /hatua (Jack anatembea), hatua (Jack, halafu Jenny, anaondoka)*

**Jack:** *(Jack anatembea na kumgusa kwa nguvu Jenny begani kutaka tu kuwaudhi watu)*'Ungali ndotoni,au? Kwa kukutazama tu ---unawaza na kutabasamu peke yako--- huwezi kuwa unafikiria kazi ya hesabu ya kufanyia nyumbani! La! Nadhani najua kinachoendelea *(kimzaha).*

“Mabibi na mabwana, mbele yenu ni binti Jenny!, na ingawa ameketi tu kwenye fomu, yuko katika tamasha ya Kofi Olomide na anakaribia kuvutwa jukwaani, na si mwengine bali Kofi mwenyewe katika mazingara ya kimapenzi...'”

**Jenny:** *(anamkatiza Jack kwa hasira, anahisi tahayuri)*
'Wacha yako wewe Jack! Wacha kunichongoa! Unayosema si kweli.... nilikuwa nikiwaza kuhusu, ,…..kuhusu,. oooh Mungu wangu!, nilikuwa nikiwaza kuhusu....

Jack: *(akiongea huku akicheka)* ' Basi tuambie, ulikuwa unawaza nini? Hali ya hewa? ..utakula nini leo usiku? … Au jambo tofauti kabisa?. Labda ulikuwa unawaza kuhusu matokeo ya mchezo wa kandanda...'

**Jenny:** *(akiwa amekasirika)*
'Sawa, sawa, wee mpumbavu. Nilikuwa nawaza kuhusu Kofi Olomide, lakini usifikiri kuwa ni mimi tu hapa anayeota---hebu jitizame macho yako jinsi yanavyong'ara unapotoka kucheza kandanda na kushangiliwa na mashabiki wako wote wasichana!'

**Jack:** *(akiwa ameshangaa na kujitetea)* 'Unasema nini wewe? Macho yangu hayang'ari hata. Asilan! Sio kwa sababu ya mtu yeyote, na hasa wasichana. Nini wewe?'

**Jenny:** 'Labda unampenda mtu?'

**Jack:** 'Upuzi huo! Wewe ndiye unayependa mtu!.. Sio mimi! Unasema nini wewe? Nakwenda zangu.Siku njema.'

*(hatua zikiondoka)*

(*aongea pekee huku akiondoka)* 'Anaongea juu ya nini? Hata mapenzi ni nini?'

**Jenny:** *(anamuita Jack huku akiongea pekee)* 'Jack? Jack! Subiri. Nini mbaya na huyu? Amenikasirikia? Nini mbaya na sisi?...tunaongea kuhusu mapenzi na Jack hata hataki kusikiliza huku akifikiri mimi nampenda Kofi Olomide,…. upuzi mtupu!. Mtu hujuaje yuko kwenye mahaba? Mepenzi yemekuweko tangu jadi? ..Na mtu hujisikiaje? Ooh Mungu wangu sijui kitu---Nitamuuliza nyanyangu anielezee kuhusu

swala hili....'

*(hatua zikiondoka)*

**Scene 2**

*Sherehe za familia, watu wengi wakiburudika, muziki, hatua (Nele anakuja mbio)*

**Jenny:** (kando kidogo, akiongea pekee) 'Agh, Balaa gani hii--- familia yote iko apa kusherehekea! Nilitaka kuwa peke yangu na nyanya nimuulize kuhusu upuzi huu unaoitwa mapenzi..'

*(hatua zikikaribia)*

**Nele:** *(msichana mdogo anakuja mbio na kuushika mkono wa Jenny}*'Njooo Jenny, njoo, nyanya anatuhadithia ya kale, njoooo!

**Jenny:** *(akiwa na hasira)* 'Nele wewe una umri mdogo wa miaka saba, na mimi 14. Unaelewa? Mimi si mtoto tena kusikiliza hadithi za kale.'

**Nele:** 'Hapana, wewe si mzee, nataka uje usikilize. Nyanya anatuhadithia kuhusu mapenzi ya binti ya mfalme na......'

**Jenny:** 'Sawa. Sawa, naja. Kwa vile ni hadithi ya mapenzi...'

*(Wanaandamana kwenda kwa nyanya yao)*

**Nyanyake Jenny:** (*akitoa hadithi ya mapenzi, na wasichana hao wawili wakiungana na watu wengine wanaosikiliza)* '...na halafu huyo mfalme akaamua kwamba bintiye mrembo Adetola apaswa kuolewa, na Adetola akakubaliana na babake, ambaye alisema 'Nataka kukutafutia mume atakayekuoa sio kwa sababu ya urembo na utajiri wako bali kwa sababu anakupenda kwa moyo wake wote.' Mfalme huyo akawaita mabaro-baro wote katika nchi yake wafike nyumbani kwake. Na wote walikuja na zawadi nono nono --- kila mmoja akiwa na nia ya kumpata Adetola kuwa mke wake. Hata hivyo mmoja wao hakuleta zawadi nono ---alileta bangili tatu tu kwa sababu alikuwa masikini. Lakini alipomuona Adetola, macho yake yalijaa machozi kwa sababu alikuwa mrembo na kumpenda sana. Baada ya kuwaona vijana hao wote, Adetola hakuweza kuamua yupi anampenda....alikwenda kulala ili amshauri babake siku iliyofuata.Usiku huo, Adetola aliota kuhusu marehemu mamake, ambaye alimpa ushauri. Alimwambia 'Adetola kama wataka kweli kujua anayekupenda zaidi, mwambie babako atangaze kuwa wewe ulifariki wakati wa usiku. Na Kutokana na jinsi watakavyopokea habari hizo, utaweza kujua ni yupi anakupenda zaidi!.' Siku

iliyofuata Adetola alimwambia babake kuhusu hiyo ndoto yake na wakaamua kutekeleza mpango huo. Mfalme aliwaambia vijana hao waliokuja kuchumbia binti yake kwamba amefariki usiku huo. Wengi wao walionekana wenye huzuni kwa muda mfupi, lakini baadaye walifunga virago vyao na kuondoka kutoka jumba la mfalme. Hata hivyo, mmoja alibakia, moyo wake ukiwa umefunikwa na wingu la huzuni. Yule kijana aliyeleta zawadi za bangili tatu alimpenda sana Adetola hivi kwamba aliangua kilio punde tu kusiki kifo Adetola. Na hivyo ndivyo uamuzi ulivyofanwa. Kijana huyo, ambaye aliitwa Alaba, alimuoa Adetola na maharusi hao wawili waliishi raha mustarehe maisha yao yote....*(Nyanya anawatazama wasikilizaji wake)* Si hiyo ni hadithi nzuri, wajukuu wangu? Jenny, wewe pia ulikuwa ukinisikiliza? Kwani unalia?'

Jenny: *(akiwa ametahayari, anakama pua na kuongea kama aliye changanyikiwa)* 'Hapana silii. La hasha! Ni vile tu ilikuwa hadithi nzuri na kila kitu wakati huu kinaonekana kuwa ni kuhusu mapenzi na ... sijui nahisi vipi tumboni mwangu... huu ubishi nilikuwa nao na Jack...hata hivyo asante nyanya, kwani hujui ni vipi au kwa nini lakini umenisaidia sana.'

**SCENE 3**

*mlango unabishwa, mlango unafunguliwa*

**Tom:** (*anabisha na kuingia chumbani kwa fujo, akiwa na furaha)* 'Habari ya asubuhi! Amka, amka. Wakati umewadia wa kuamka ndugu, amka, amka.
****

*(shuka zikungutwa)*

**Jack:** *(anajificha chini ya shuka na hana raha)*
'Fujo ya nini ? Kwa nini unaniamsha? Sitakwenda shule leo!'

**Tom:** 'Kwa hivyo? Hiyo si sababu ya kulalahadi saa sita! Nadhani itakusaidia ukitoka nje kidogo. Umebadilika sana katika siku za hivi punde, sikuelewi!. Si uniambie kinachoendelea.'

**Jack:** *(akinong'ona ndani ya shuka)* 'Ajabu, kaka anaelewa kila kitu! Kwa kweli sina raha.Naudhika nakitu kidogo siku hizi . Nadhani ni mgonjwa.'

*(mtu anaketi kitandani)*
**Tom:**'Subiri kidogo, fungua hizi unazojifunika....Ni nini mbaya?'

*(mtu anasukuma shuka na kuinuka)*

**Jack:** *(anasukuma shuka na kuketi kitandani...anaongea haraka na kwa hasira)*
'Oh, kwa kweli sijui.....kila kitu kina makosa....mimi na Jenny tumekuwa na ubishi na kuhusu mapenzi na wapendanao...'

**Tom:** *(kwa mshangao)* 'Subiri kidogo, sijui kama nimekuelewa? unampenda?

**Jack:** *(kwa hasira)* 'Sasa usiniletee. La, sina mpenzi. Na kama ningelikuwa naye inapasa kwanza nijui mapenzi ni nini. Hakuna mtu ananieleza maana ya mapenzi.Kwangu naona kama ugonjwa.'

**Tom:** *(anapumua na kuegemea nyuma)* 'Sasa naona wakati umewadia tuzungumze kama wanaume. Kupitia utafiti wangu wa muda mrefu kuhusu hisia za mapenzi nimegundua *(anacheka)* la, la, si jambo la mzaha! kwa kweli hujakosea kuhusu hii hisia ya ugonjwa...nitakwamba jambo moja na usimwambie YEYOTE, unasikia? Niahidi hutamwambia mtu!'

**Jack:** 'Ndio, naahidi sitamwambia mtu!'

**Tom:** 'Sawa, mara ya kwanza nilihisi mapenzi nilikuwa na umri kama wako...sikujua kilichokuwa kikiendelea. Nilikuwa nasikia vibaya na kila nilipomuona Dina nilijihisi mgonjwa..'

**Jack:** *(anaangua kicheko)* DINA? Dina huyu jirani yetu?'

**Tom:** (*akiudhika kidogo, lakini halafu anamudu hisia zake)*
'Ndio, ni Dina huyo huyo. Nyamaza, au niach kukueleza! Hivyo basi kila nilipomuona nilihisi hali nisiyojielewa. Na hata nilikwenda kumuona daktari kuhusu hali hiyo *(Jack anacheka)* kwa sababu maradhi hayo yalikuwa hayamaliziki na kuumwa na kishwa. Huyo daktari alicheka kama vile wewe tu na kuniambia mahaba yalikuwa yakinisumbua . Alisema hali hiyo husababishwa na homoni. Alisema hizo homoni ndizo zinazoleta mabadiliko ya kutoka ujana na kuingia utu uzima. Na alisema ni wakati huo ambapo wavulana huanza kutamani wasichana na wasichana kuwatamani wavulana au vijana wa jinsia moja. Hata hivyo, yeyote unayempenda, hali hiyo inapotokea, mwili hutoa homoni inayoitwa adrenalini, na hiyo ndiyo hukufanya ujihisi mgonjwa, hasa unapomuona msichana. Au kuhisi joto kichwani. Alisema hilo ni jambo la kawaida. Ingawa mtu anahisi kama ugonjwa, lakini si ugonjwa.akasema hivyo Daktari na mimi nilimuamini. Halafu baada ya muda fulani, sikujihisi tena mgonjwa....nilijihisi sawa na nilijuwa kuwa wale wengine pia walihisi kama mimi. Na hivyo ndivyo ilivyo. Jack? Unanisikiliza kweli?'

**Jack:** *(akiwa na tahayuri)* 'Ndio kaka...nakusikiliza na naelewa unamaniha nini. Asante kwa kunielimisha. Nadhani nina hali kama hiyo, lakini haihusiani na wale wasichana wanaokuja kutazama kandanda bali ni mtu mwengine. Nahitaji muda wa kutafakari lakini wache nitatoka nje. Tufanyeje sasa ?'

**Tom:** *(akiwa na raha)* 'Ahaa, sasa umerejea katika hali yako ya kawaida. Twende basi.'

Jack: *(akisita)* 'Hebu subiri kidogo! Nimekumbuka kitu. Tukutana baadaye.'

**Tom:** 'Sawa, lakini fanya haraka, nitakungojea nje.'

*(hatua za Tom akiondoka, mlango unafungwa)*

Jack: 'Nadhani nahitaji kumuona mtu kwa dharura.'

(*akituma ujumbe kupitia kwa simu ya mkono)* " Ah Jenny, vipi sasa? Unaweza kuja uwanjani? Jack" Tuone kama atakuja..'

*(mlango unafungwa)*

**Scene: 4**
*(mchezo wa kandanda)*

**Tom:** *(akipiga kelele)* 'Jack, unafanya nini? Mbona unacheza vibaya hivyo leo? Mbona huangalii mpira? JACK, Mungu wangu! Mbona unaangalia barabarani mara kwa mara? Unamtarajia mtu?'

**Jack:** *(anahisi amegunduliwa)* 'Hapana, naa ...nacheza.......JENNY!!!!'

**Jenny***: (akipiga ukelele kwa mbali)* 'Wee, Jack! Jack? Chunga, geuka, mpira unakuja!!!'

*(mpira unagonga kichwa cha Jack)*

**Jack:** 'Ooowu!!'

*(Jenny anakuja mbio)*

**Jenny:** *(akiwa na wasi wasi)* 'Jack, uko sawa?'

**Jack:** 'Ndio, niko sawa. Nimefurahi kukuona.'

**Jenny:** 'Hata mimi pia. Na nimejifunza mengi kuhusu mapenzi na wanpendanao, lakini haihusiani na kumhusudu mwimbaji au bendi...!'

**Jack:** '....na haihusiani na wasichana wanaotazama kandanda! Lakini kwa kweli ni kama ugonjwa ..'

**Jenny**: 'Ndio, kama ule ubishi tuliokuwa nao....'

**Jack:** 'Ni jambo la kawaida kabisa...kama kuwa mtu mzima!'

**Jenny:** 'Na wakati mwingine ni kama hadithi....na dalili zake ni hisia ya kumtamani mtu na kutaka kuwa karibu naye daima...'

**Jack:** 'Ndio, hiyo ni kweli. Ni kumtamani mtu na kutaka daima muwe pamoja.'

**Jenny:** 'Ah, wacha yako, Jack. Sasa unaanza kuwa mtundu...'

**Jack:** 'Unasema kweli, lakini mimi pia nasema kweli. Sasa ningependa tuwe pamoja kila wakati..'

**Jenny:** 'Ndio. Nasikia raha sana!'

Muziki

OUTRO (Mtangazaji)

Na sasa ni nini kilichosalia? Hawa watu wawili, Jenny na Jack, wataendelea kuishi pamoja daima? Labda unaweza kutunga mwisho wa hadithi hii. Na hiyo ndiyo makala ya mwisho ya Tega Sikio ujifunze , Elimu ya Kawaida'. Makala hii maalum kuhusu mapenzi imeandikwa na Christine Watty. Pia unaweza kusikiliza yote tuliyojifunza kuhusu sayansi wakati wa mfululizoa vipindi vyetu kupitia mtandao www.dw.de/kiswahili. Asante kwa kutusikiliza na furahia safari yako ya kimapenzi!